## Maswali

1 . Malaika watatu walipea Ibrahimu na Sara habari gani njema?
2. Ibrahimu na Sara walimwita mwanao eti nani?
3. Mungu alitaka Ibrahimu afanye nini?
4. Ibrahimu na Isaka walisafiri kwenda wapi?
5. Isaka alibeba nini wakienda mlimani?
6. Isaka aliuliza Ibrahimu nini? Ibrahimu alijibu nini?
7. Huko mlimani Ibrahimu alifanya Isaka nini?
8. Malaika alimwambia Ibrahimu nini?
9. Ibrahimu alimtolea Mungu nini badala ya Isaka?
10. Mungu alimwaahidi Ibrahimu nini?

## Majibu

1. Malaika waliwambia kwamba watapata mwana.
2. Walimuita mwanao Isaka.
3. Mungu alitaka Ibrahimu auwe Isaka kama dhabihu.
4. Ibrahimu na Isaka walisafiri kwenda mlima wa Moria.
5. Isaka alibeba kuni mpaka mlimani
6. Isaka aliuliza Ibrahimu alikokuwa mwana kondoo. Ibrahimu alisema, Mungu atapeana.
7. Ibrahimu alimfunga Isaka, akamweka kwenye madhabahu na akainua kisu chake ili amuuwe.
8. Malaika alimwambia Ibrahimu asimuuwe Isaka.
9. Ibrahimu alimtolea Mungu kondoo ndume badala ya Isaka.
10. Mungu alimwaahidi Ibrahimu uzao mwingi kama nyota au mchanga – hawahesabiki. Mzao wake mmoja atabariki mataifa yote.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2    Mwaka wa 1

# 6 Isaka kama dhabihu

**Kwa Biblia** Mwanzo 18:1 – 11 na Mlango wa 22

### Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu alitimiza ahadi zake kwa Abramu. Abramu alimtii Mungu. Mungu alifurahia imani ya Abramu.

### Somo

Mungu alifanya ahadi za kipekee kwa Abramu. Moja ya hizo ahadi ni kwamba Abramu na Sarai watapata mwana. Abramu na Sarai walingoja kwa miaka mingi .Wakawa wezee lakini hawakupata mwana.

Siku moja Mungu alimzungumzia Abramu tena. Mungu alizirudia hizo ahadi. Mungu alibadilisha jina la Abramu na akamuita IBRAHIMU. Akabadilisha la Sarai likawa SARA .Hii ilikuwa ishara kwamba Mungu atatimiza ahadi zote.

Baadaye, Ibrahimu alikuwa amekaa kwa hema yake amejikinga jua. Aliona wanaume watatu wakija. Alikimbia kuwakutanisha. Akawalaki wale wanaume watatu. Aliwapeleka wakae chini ya mti wa mwaloni. Aliwaosha miguu kwa maji baridi.

Kwa haraka Sara alitengezea wale watu watatu chakula. Ibrahimu na wale watu walikaa chini ya mwaloni na kukula.

Mmoja wa wale watu aliuliza, “Wapi Sara mkeo?”
“Ako hemani,“ Ibrahimu alijibu.
Yule mtu akasema, “Mwaka ujao Sara atakuwa na mwana.”

Hapo Ibrahimu akakundua kwamba hawa watu ni malaika. Wameleta huu ujumbe kutoka kwa Mungu.

Ibrahimu na Sara waliposikia kwamba watapata mwana walifurahi sana. Miaka mingi ilikuwa imepita tangu Mungu aahidi kwamba watakuwa na vizazi vingi. Sasa Sara alikuwa mzee sana hangeweza kupata watoto. Lakini Ibrahimu na Sara waliamini Mungu na walisubiri kwa utulivu. Walijua kwamba hakuna lisilowezekana kwa Mungu.

Hadimae, Sara alimzaa mwana. Walimwita ISAKA. Walifurahi sana. Isaka alikua akawa mtu wa nguvu na hiyo ilikuwa furaha kwao.

Mungu alijaribu upendo na uvumilivu wa Ibrahimu tena. Siku moja Mungu akamwambia Ibrahimu, “Chukuwa mwanao, mwanao wa pekee Isaka, unayempenda. Enda kwa nchi ya Moria, kuna mlima nitakayokuonyesha. Kule lazima umuuwe Isaka ili unitolee kama sadaka ya kuteketeza.”

Ibrahimu hakufurahia. Angeuaje mwanawe wa pekee? Isaka alikuwa ameleta furaha kwake. Alikuwa ameongoja kwa mda mrefu ili Isaka azaliwe. Ahadi za Mungu zitawekwaje ikiwa Isaka atakufa?

Lakini Ibrahimu alipenda Mungu sana. Alipenda Mungu zaidi ya wote. Ibrahimu aliamini kwamba Mungu anajua yote. Alitii Mungu. Ibrahimu aliamka asubuhi na mapema. Alitayarisha punda wake. Alichukuwa watumishi wawili, kuni chache,moto na kisu.Akaondoka pamoja na Isaka.

Ibrahimu alisafiri kwa siku tatu na baadaye akafika kwa mlima wa Moria. Aliwambia watumishi wake wakae pale chini hali yeye na Isaka waende juu ya mlima ili wamuabudu Mungu halafu warudi.

Ibrahimu aliamini kwamba Mungu anaweza hata kumfufua Isaka kutoka kwa wafu.

Ibrahimu alimpa Isaka kuni abebe. Walipokuwa wakikwea mlima, Isaka aliuliza, “Babangu, tuna kuni na moto, lakini wapi mwana kondoo tutakayetoa kama sadaka ya kuteketeza?”

Ibrahimu alijibu, “Mwanangu, Yeye Mungu mwenyewe atapeana mwana kondoo wa kuteketeza.”

Walipofika pahali palipochaguliwa Ibrahimu alijenga madhabahu. Akaweka kuni juu ya madhabahu. Akamfunga Isaka. Isaka alikuwa mdogo na wa nguvu, angetoroka. Lakini alimtii babake. Ibrahimu akaweka Isaka kwenye madhabahu. Aliinua kisu amuuwe Isaka.

Papa hapo alisikia sauti ikimwita, “Ibrahimu! Ibrahimu!” Malaika alimwambia Ibrahimu. “Usimuuwe Isaka. Sasa najua kwamba unamwogopa Mungu, kwa sababu haukujizuia na mwanao wa pekee.”



Ibrahimu alijawa na furaha. Mungu amemwachilia Isaka! Ibrahimu aliona kondoo ndume ameshikwa pembe kwa kichaka. Alimfunguwa Isaka halafu akachukuwa kondoo na kumtolea Mungu sadaka badala ya Isaka.

Ibrahimu alionyesha upendo na utiivu kwa Mungu. Aliamua kumtolea Mungu hata mwanawe wa kipekee. Mungu alifurahia Ibrahimu sana. Mungu alirudia hizo ahadi kwa Ibrahhimu tena. Mungu aliahidi kumbariki na kumpa Ibrahimu uzao mwingi. Uzao wa Ibrahimu utakuwa mkubwa hata hautasabuliwa – kama nyota angani na mchanga katika pwani. Mzao wake mmoja atabariki mataifa yote ya dunia.

Ibrahimu alifurahi kwa sababu mwanawe Isaka alikuwa hai. Mungu alimpa ahadi maalumu na za dhamana.